



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI



## TANGAZO

04/06/2022

**ZABUNI YA KUTOA HUDUMA YA ULINZI KWA MAENEYO AMBAYO YAMEKUWA YAKILINDWA NA WALINZI WA MIKATABA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023.**

Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali inakaribisha maombi ya zabuni kwa ajili ya Ulinzi kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 kutoka kwa wazabuni wenye sifa za kufanya kazi hiyo

**Eneo la ulinzi ni; -**

- a) Ofisi ya Makao Makuu ya Halmashauri
- b) Ofisi za Mamlaka ya Mji Mdogo Rujewa
- c) Hospitali Mpya Wilaya
- d) Hospitali ya zamani Wilaya

### MASHARTI YA MAOMBI

1. Mwombaji awe na leseni hai ya biashara, TIN, Hati ya usajili, Utambulisho wa kisheria (Power of Attorney) na pia awe na ofisi inayotambulika (Ataje Ofisi ilipo, Anwani, Namba ya simu, Email na Fax kwa ajili ya mawasiliano).
2. Mshindi atapewa mkataba wa kisheria utakaokuwa na masuala yote muhimu ya kuzingatia katika shughuli hiyo ya ulinzi
3. Mzabuni atatumia mfumo wa kielektroniki kukili mapokezi ya fedha ,
4. Waombaji wanaweza kuwa Makampuni, Mashirika au Vikundi vya watu waliosajiliwa kisheria.
5. Mwombaji haruhusiwi kuweka alama yoyote ya utambulisho wake juu ya bahasha.
6. Mwombaji aambatanishe idadi ya mikataba ya kazi na vielelezo (kama vile baruu ya kuteuliwa kuwa mzabuni, Fomu ya makubaliano ya mkataba) alizowahi kufanya .
7. Mwombaji Atatuma maombi, Juu ya bahasha iandikwe kwa **HERUFI KUBWA** na zabuni ifungwe kwa **LAKIRI (Seal)** na maombi yakiambatana na kivuli cha stakabadhi ~~ya~~ ada na maombi yatumwe kwa,

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI,  
S.L.P 237,  
RUJEWYA – MBEYA.**

8. Vitabu vya zabuni kwa lugha ya kiswahili vinauzwa kwa **Tshs.100,000/=** ambazo hazitarudishwa kwa mwombaji na vinapatikana katika ofisi ya Afisa Ugavi (W), **Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, S.L.P 237, RUJEWYA –MBARALI.**
9. Malipo yafanyike kupitia Benki ya NMB, Akaunti ya **Own Source Collection**, Akaunti namba **6110000719** baada ya kupewa **Control Number** kutoka kwa **mhasibu wa Halmashauri** na slip ya bank iletwe kwa mhasibu ili kupatiwa risiti kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 09:30 alasiri siku za kazi.
10. Maelezo ya ziada (masharti) yanapatikana kwenye kitabu cha zabuni husika.
11. Bodi ya zabuni ya Halmashauri ya wilaya ya Mbarali hailazimiki kukubali au kukataa ombi lolote.

12. Mwombaji anashauriwa kabla ya kuomba zabuni yoyote kufanya utafiti wa kutosha.
13. Mwombaji anaweza kuja ofisi za Halmashauri kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kupata ufanuzi atakaohitaji ikiwa ni pamoja na kuonyeshwa maeneo ya kazi.
14. Mwisho wa kuwasilisha maombi ni 14/06/2022 saa 5:00 asubuhi na zabuni zitafunguliwa siku hiyo saa 5:01 asubuhi katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya. Waombaji au wawakilishi wao wanakaribishwa kuhudhuria siku ya ufunguzi.



Jabir A. Makombe,

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)

**MBARALI.**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
MBARALI

---

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Mtaa wa Mpungarelini, S.L.P 237, Rujewa.  
Simu 252957440/252957447, Nukushi 025-2590089/2590108, Barua pepe: [ded@mbaralidc.go.tz](mailto:ded@mbaralidc.go.tz),  
[info@mbaralidc.go.tz](mailto:info@mbaralidc.go.tz), Tovuti: [www.mbaralidc.go.tz](http://www.mbaralidc.go.tz)